

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI VETA



NGORONGORO DVTC

S.L.P. 1 LOLIONDO, ARUSHA

## KUJIANDIKISHA KOZI YA USINDIKAJI BIDHAA ZA MIFUGO

### (MAZIWA NA NGOZI)

CHUO CHA VETA NGORONGORO kimeandaa Mafunzo kwa Wananchi ya Usindikaji bidhaa za Mifugo kama Maziwa na Ngozi pamoja na Ujasiriamali. Mafunzo yatafanyika Chuo cha VETA NGORONGORO kilichopo katika Kijiji cha Samunge Wilayani Ngorongoro, Kata ya ~~SALE JANUNGE~~ (Karibu na kwa BABU WA KIKOMBE).

Mafunzo hayo yatatolewa kwa Ufadhili wa Serikali Kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa kushirikiana na VETA ambapo Ufadhili huu utagharamia ADA TU kwa Mshiriki kwa mafunzo yote.

Mafunzo haya yatamuwezesha Mshiriki kufahamu misingi na hatua sahihi za usindikaji wa bidhaa za mifugo (maziwa na ngozi) na pia mbinu za kufanya biashara ya bidhaa hizo.

Mshiriki atakayehudhuria mafunzo hadi mwisho atapatiwa cheti cha ushiriki.

Ili uweze kushiriki Mafunzo haya, unaombwa Kujaza fomu hii ikiwa ni hatua ya awali ya Kuleta na Kupokelewa maombi yako. Hatua nyingine zitafuata pamoja na kujulishwa tarehe ya kuanza mafunzo.

NB: Taarifa unazojaza kwenye fomu hii ni kwa ajili ya matumizi ya kiofisi tu, hazitawezza kusambazwa kwa mtu au taasisi yoyote kwa matumizi tofauti na mafunzo haya.

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

KANDA YA KASKAZINI (KILIMANJARO, ARUSHA NA TANGA)



PROGRAMU YA MAFUNZO KWA WAFUGAJI WILAYA YA NGORONGORO - LOLIONDO,  
SAMUNGE

FOMU YA USAJILI WA WASHIRIKI WA MAFUNZO 2020

1.	JINA LA MSHIRIKI			
	JINSIA YAKO	UMRI	MWANAUME	MWANAMKE
2.	JINA LA KIJIJI UNACHOTOKA NA ANWANI			
3.	JINA LA KIKUNDI			
4.	NAMBA YA/ZA SIMU			
5.	KIWANGO CHA ELIMU			
6.	MAFUNZO ULIYOWAHI KUPATA			
7.	TAFADHALI ELEZEA KAZI UNAZOFANYA KWA SASA			
8.	MATARAJIO BAADA YA MAFUNZO			
9.	SAHIHI			
10.	TAREHE			
KWA MATUMIZI YA OFISI TU				